- UTANGULIZI

Eneo kubwa la jamii yetu kwa sasa hasa ukizingatia na kulinganisha na takwimu mbalimbali zinazotokana na tafiti mbalimbali, zinaonyesha kuwa jamii zetu na dunia kwa ujumla zinazungukwa na idadi kubwa ya wanawake. kutokana na tafiti hizi bila kupepesa macho tunagundua kuwa ipo haja ya kuwekeza maarifa na taarifa sahihi ndani mabinti na wanawake kwa ajili ya ustawi na usalama wa jamii zetu na dunia kwa ujumla. Hiyo inatujulisha kuwa ipo haja ya kuhakikisha mabinti hawa wanajengwa kwa maarifa sahihi kwani ndio watakaokuwa wake za watu, mama na walezi kwa watoto wetu.
Ili haya yote yaweze kufikiwa kwa ufanisi mkubwa bila shaka ni lazima mabinti waweze kujengwa kwa maarifa sahihi yanayotokana na neno sahihi la Mungu.Jambo jingine lililonipa kiu na shauku ya kuandika kitabu hiki ni msisitizo uliopo kwenye maandiko kuhusiana na nyakati tulizonazo;

- JAMBO LA 1:
  Tunaishi Kwenye Dunia Inayolewa-Lewa Na Kuwaya-Waya

  Isaya 24:20
  Dunia inalewa-lewa kama mlevi, nayo inawaya-waya kama machela; na mzigo wa dhambi zake utailemea; nayo itaanguka, wala haitainuka tena.

Kufuatana na msisitizo wa andiko hili, na sote tunajua Mungu anaposema dunia inawaya-waya au kulewalewa anazungumzia wanadamu waliopo ndani yake kulewa-lewa au kuwaya-waya, natumai sote tumewahi kusikia msemo usemao ya kuwa dunia sio mbaya ila

wanadamu ndio wabaya au ndio wanaoifanya dunia kuonekana ni mbaya na pasiwe mahali salama pa kuishi.

Kutokana na mtazamo huu, Roho mtakatifu aliniwekea msisitizo wa kuandika kitabu hiki kwa ajili ya kuinua jeshi la wanawake wamchao Bwana katikati ya kizazi hiki kiovu. Ile kwamba tunaishi kwenye dunia hii inayowaya-waya na kulewa-lewa, bado haitupi kibali na sisi kuingia kwenye kundi la wanaolewa-lewa na kuwaya-waya! Ninachojua ni kwamba kwa neema ya Mungu bado kuna wanawake wanaoweza kuishi kwa ushindi kinyume na mapenzi ya dunia hii!

➢ JAMBO LA 2:
Tunaishi Kwenye Nyakati Zilizoratibiwa Kwa Ajili Ya Uovu

Waefeso 5:15-17
Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; Mkiukomboa wakati kwa maana ZAMANI HIZI NI ZA UOVU.Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana.

Maandiko yanazungumza kwa kutambulisha moja ya kipindi ambacho kwa sasa tunaishi ndani yake, maandiko yanakiita ZAMANI ZA UOVU; hiki ni kipindi ambacho kimebeba uovu ndani yake, ni kipindi ambacho hakisapoti mambo ya kiUngu kabisa. Sasa kuna kitu ambacho Paulo anakizungumza katika mstari wa 17; anasema kwa sababu tunaishi kwenye zama hizi za uovu, zama ambazo ushoga na usagaji vinapigiwa debe kwa mwamvuli wa haki za binadamu, zama ambazo zimejaa maasi ambayo inawezekana hata shetani mwenyewe wakati mwingine huwa anashituka yanapovumbuliwa; bado hatupaswi kuenenda kama wajinga!

Bali tunapaswa kufahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Mungu katikati ya kipindi hiki.

Sio suala la kulalamika kuwa maasi yamezidi kila mahali, ni suala la sisi kufahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Mungu kwa sababu tupo kwenye kipindi hiki tayari, kulalamika ni ishara ya kwamba hatujui cha kufanya, na tunaposhindwa kujua yatupasayo kufanya bila shaka hatutakwepa kuenenda kama wajinga na kama tutaenenda kama wajinga bila shaka hatutakwepa kuenenda kama dunia inavyoenenda. Ahimidiwe Mungu aliyetupa neema ya kuandika kitabu hiki kwa ajili ya kumsaidia binti walau mmoja kuishi sawa sawa na mapenzi ya Mungu katikati ya nyakati hizi hizi za uovu.

➢ JAMBO LA 3:
  Ni Mwanamke Pekee Amchaye Bwana Ndiye Atakayeweza Kuishi Maisha Ya Ushindi Katikati Ya Nyakati Hizi

  Mithali 31:30
  Upendeleo hudanganya, na uzuri ni ubatili; BALI MWANAMKE AMCHAYE BWANA NDIYE ATAKAYESIFIWA.

Moja ya kundi rika linalokumbwa na changamoto nyingi katika nyakati hizi ni kundi la mabinti! Leo si ajabu kusikia binti mdogo akitembea na mzee wa umri ambao ni sawa na baba yake! Sio ajabu kusikia mabinti wakiangukia kwenye tabia sugu kama ukahaba, uraibu wa madawa ya kulevya, shisha n.k, yote haya ni matokeo ya ukosefu wa maarifa na taarifa sahihi kwa ajili ya kuweza kuwasaidia kuvuka eneo hili la ujana kwa ushindi.

Moja ya jambo muhimu linaloweza kumsaidia binti kuishi maisha ya tofauti na yenye ushindi dhidi ya dunia hii iliyobeba makusudio mbalimbali; NI KWA KUMCHA MUNGU ALIYE HAI. Na kumcha Mungu ni matokeo ya binti kuwa na maarifa sahihi kuhusu eneo hili.

Kwa neema ya Mungu kitabu hiki kipo mkononi mwako kwa ajili ya kuachilia maarifa sahihi kwa mujibu wa neno la Mungu.Kusudi kubwa la kitabu hiki ni KUZALISHA MABINTI WENYE UTOFAUTI NA MGUSO WENYE MATOKEO CHANYA KATIKATI YA KIZAZI HIKI.

- Ni maombi yangu kwa Bwana, kila binti anayesoma kitabu hiki akapate kujengwa na kuwa binti wa tofauti na mwenye mguso wenye matokeo chanya katikati ya kizazi hiki. Dunia tunayoishi inazungukwa na watu wenye miguso ya aina mbalimbali, shabaha ya kitabu hiki ni kuinua mabinti wenye mguso chanya, haitoshi wewe kuwa na mguso; SUALA NI AINA YA MGUSO HUO.

Mungu aliyenipa neema ya kuandaa kitabu hiki kwa msaada wa Roho mtakatifu; ninaamini kuna maisha ya mabinti wengi yanaenda kuguswa na kubadilishwa kwa namna ya tofauti kabisa.

Ninakualika sasa upate kufuatana na mimi katika kitabu hiki na neema ya Mungu ipo tayari kwa ajili ya kuhudumia maisha yako na kuyageuza jumla kwa msaada wa Roho mtakatifu.

KARIBU SANA.